**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA MFAMASIA DUNIANI TAREHE 25 SEPTEMBA, 2022

**Dodoma, 25 Septemba, 2022**

Siku ya Mfamasia Duniani huadhimishwa kila mwaka Tarehe 25 Septemba. Siku hii ilianza kuadhimishwa mwaka 2009 na *International Pharmaceutical Federation Council* (FIP) kwa dhumuni la kusaidia kujitolea kupanga shughuli ambazo zitakazokuza na kuunga mkono jukumu la mfamasia katika kuboresha afya duniani kote.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Mfamasia Duniani kwa mwaka huu ni "**Pharmacy united for healthier world**"- kwa tafsiri ya "**Mshikamano katika huduma za famasi kwa dunia yenye ustawi wa afya**".

Ujumbe huu unaeleza kwamba wataalamu wa kada ya famasi wakiwemo wanasayansi wa dawa na wengine ambao ni sehemu ya fani hii ambapo takribani watu milioni nne wanajihusisha na taaluma hii duniani kuwa mshikamano katika utendaji wa taaluma (pharmacy practice).

Wote tunatambua kuwa Wataalamu wa kada ya Famasi (Wafamasia) ni sehemu muhimu katika timu ya huduma za afya zinazo saidia kuwafanya watanzania kuwa

kufanya hivyo katika kutoa elimu ya Afya na dawa, kutoa ushauri na kurahisisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa wahitaji.

Napenda kuwakumbusha wafamasia wote nchini, wanapoadhimisha siku ya Mfamasia Duniani, kwamba usimamizi wa bidhaa za afya ikiwemo dawa ni suala la usalama wa Taifa. Zaidi ya asilimia 50 ya matumizi ya sekta ya afya nchini yanaenda katika eneo hili. Hivyo ni wajibu wa wafamasia kuwa mstari wa mbele kusimamia upatikanaji, usambazaji, uhifadhi na matumizi sahihi ya bidhaa hizi ili kuleta tija ya uwekezaji mkubwa wa Serikali katika eneo hili.

Hata hivyo tunafahamu kwamba, wafamasia wenye weledi ni muhimu sana katika sekta ya afya, na kwa sasa kuna ongezeko kubwa la wahitimu wa taaluma hii ya Famasi nchini, hivyo niwatake watoa huduma za afya kote nchini kuhakikisha maeneo yote yanayohusu dawa yanasimamiwa na wataalamu wa kada ya Famasi ili kulinda usalama wa afya za watanzania hasa kwa kuzingatia kaulimbiu ya siku ya usalama wa mgonjwa Duniani 17 Septemba 2022, iliyosema "**Usalama wa matumizi ya dawa-Dawa bila madhara**"

Wafamasia mnakumbushwa kuzingatia maelekezo mnayopewa mara kwa mara na Wizara ya afya ikiwemo kuzingatia mwongozo wa Matibabu na Orodha ya Taifa ya dawa muhimu (STG/NEMLIT) ili kuhakikisha huduma bora kwa wananchi zinatolewa kwa kuzingatia miongozo iliyopo na kuendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya dawa ili kuleta matokeo yaliyokusudiwa na kupunguza usugu wa vimelea dhidi ya dawa (antimicrobial resistance) na kupunguza gharama za matibabu.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wataalamu wote wa kada ya famasi kwa kujitoa kwao kuhakikisha ustawi wa afya za watanzania. Niwaombe watanzania wote kuungana nami kuadhimisha na kusherehekea pamoja na wafamasia siku hii muhimu na namna zote ambazo wanataaluma wa famasi wanaendelea kujitokeza na kuwahudumia watanzania wa makundi yote.

Limetolewa na:

Dkt. Seif A. Shekalaghe
**KAIMU KATIBU MKUU**